# Mark Scheme (Results)

Summer 2021

Pearson Edexcel International GCSE
In Swahili (4SW1)
Paper 02: Listenning

**Edexcel and BTEC Qualifications**

Edexcel and BTEC qualifications are awarded by Pearson, the UK's largest awarding body. We provide a wide range of qualifications including academic, vocational, occupational and specific programmes for employers. For further information visit our qualifications websites at www.edexcel.com or www.btec.co.uk. Alternatively, you can get in touch with us using the details on our contact us page at www.edexcel.com/contactus.

**Pearson: helping people progress, everywhere**

Pearson aspires to be the world's leading learning company. Our aim is to help everyone progress in their lives through education. We believe in every kind of learning, for all kinds of people, wherever they are in the world. We've been involved in education for over 150 years, and by working across 70 countries, in 100 languages, we have built an international reputation for our commitment to high standards and raising achievement through innovation in education. Find out more about how we can help you and your students at: www.pearson.com/uk

Summer 2021
Question Paper Log Number P66505
Publications Code 4SW1_02_2106_MS
All the material in this publication is copyright
© Pearson Education Ltd 2021

## General Marking Guidance

- All candidates must receive the same treatment. Examiners must mark the first candidate in exactly the same way as they mark the last.
- Mark schemes should be applied positively. Candidates must be rewarded for what they have shown they can do rather than penalised for omissions.
- Examiners should mark according to the mark scheme not according to their perception of where the grade boundaries may lie.
- There is no ceiling on achievement. All marks on the mark scheme should be used appropriately.
- All the marks on the mark scheme are designed to be awarded. Examiners should always award full marks if deserved, i.e. if the answer matches the mark scheme. Examiners should also be prepared to award zero marks if the candidate's response is not worthy of credit according to the mark scheme.
- Where some judgement is required, mark schemes will provide the principles by which marks will be awarded and exemplification may be limited.
- When examiners are in doubt regarding the application of the mark scheme to a candidate's response, the team leader must be consulted.
- Crossed out work should be marked UNLESS the candidate has replaced it with an alternative response.

**International GCSE in Swahili**

**Paper 2: Listening**

| Question number | Answer | Mark |
|---|---|---|
| **1(a)** | G | **(1)** |
| **1(b)** | E | **(1)** |
| **1(c)** | D | **(1)** |
| **1(d)** | A | **(1)** |

| Question number | Answer | Mark |
|---|---|---|
| | B, E | **(2)** |
| | A, G | **(2)** |
| | C, F | **(2)** |

| Question number | Answer | Mark |
|---|---|---|
| **3(a)** | Gari | **(1)** |
| **3(b)** | Kukarabatiwa<br><br>NA<br><br>Kuwa la kisasa | **(2)** |
| **3(c)** | Za kutisha | **(1)** |
| **3(d)** | Kiingilio ghali<br>NA<br>Mbali / Anaishi nje ya mji / jumba halipo karibu na nyumbani | **(1)** |

| Question number | Answer | Mark |
|---|---|---|
| **4(a)** | (a) Lola - Chanya (+) na Hasi (-) | **(1)** |
| **4(b)** | (b) Mkude – Chanya (+ ) | **(1)** |
| **4(c)** | (c) Asha – Hasi (-) | **(1)** |
| **4(d)** | (d) Chege – Chanya na Hasi (+ &-) | **(1)** |
| **4(e)** | (e) Abushiri - Chanya (+ ) | **(1)** |
| **4(f)** | (f) Kurwa– Hasi (-) | **(1)** |

| Question number | Answer | Mark |
|---|---|---|
| **5(a)** | D | **(1)** |
| **5(b)** | B | **(1)** |
| **5(c)** | D | **(1)** |
| **5(d)** | A | **(1)** |
| **5(e)** | D | **(1)** |
| **5(f)** | B | **(1)** |

| Question number | Answer | Mark |
|---|---|---|
| **6(a)** | L | **(1)** |
| **6(b)** | A | **(1)** |
| **6(c)** | B | **(1)** |
| **6(d)** | M | **(1)** |
| **6(e)** | K | (1) |
| **6(f)** | D | **(1)** |

| Question number | Answer | Accept | Reject | Mark |
|---|---|---|---|---|
| **7(a)** | Bei rahisi | Punguzo la bei | | **(1)** |
| **7(b)** | Hakuna viti | Umati wa watu | kusimama | **(1)** |
| **7(c)** | Raha / starehe | urahisi | | **(1)** |
| **7(d)** | Huleta uchafuzi wa mazingira | | | **(1)** |
| **7(e)** | Uhuru wa kusafiri | Hakuna foleni<br>Kufika haraka | kasi | **(1)** |
| **7(f)** | Hali mbaya ya hewa | kulowa | | **(1)** |

# Transcript

# Summer 2021

Pearson Edexcel International GCSE
In Swahili (4SW1)
Paper 02: Listenning

## Eneo Gani?

### Question 1

**Example**

**F1** Nilinunua tiketi ya gari moshi pale kituoni.

**Question 1 Part (a)**

**M1** Watoto hupenda kupanda miti porini.

**Question 1 Part (b)**

**F1** Mwalimu alisema tutatembelea makumbusho ya taifa wiki ijayo.

**Question 1 Part (c)**

**M1** Samaki watamu huuzwa kwenye fukwe za bahari.

**Question 1 Part (d)**

**F1** Baba atatupeleka mgahawani wiki ijayo.

## Hali ya Hewa

### Question 2

**Example**

**M1** Hannah, hivi unapendelea hali gani ya hewa?

**M2** Mimi ninalipenda sana joto na kiangazi ndiyo msimu ninaoupendelea.

**Questions**

**M2** Na wewe je Mikeli? Kuna hali ya hewa inayokuvutia zaidi?

**M1** Nchi yangu ina joto sana kwa hivyo nimezoea kuishi kwenye hali hiyo ingawa hali niipendayo ni ya baridi ambapo kunakuwa na theluji. Kama hakuna theluji basi hata mvua huniliwaza. Sauti ya matone ya mvua yanapodondoka juu ya ardhi hunifurahisha sana.

**M2** Na wewe je Lulu?

**F1** Mimi ninapenda hali ya hewa nchini kwetu. Ninapenda kukaa nje wakati upepo mwanana unapovuma. Ninapokuwa ndani ya nyumba siogopi kusikia ngurumo za radi zikipiga.

**M2** Hatimaye, Omari!

**M1** Ninapenda kutembea nje kwenye ukungu. Pia ninavutiwa na siku zenye mawingu.

## Sinema

**Question 3**

| | |
|---|---|
| **M2** | Jina langu ni Doto. Ninaishi katika mji wa Morogoro na kila wikendi mimi hupendelea sana kuenda sinema. Kwa kawaida huenda kwa kutumia gari la mama yangu, siendi kwa miguu kamwe. Jumba la sinema ni la kizamani kidogo. Ningefurahi kama lingekarabatiwa na kuwa la kisasa. Labda siku moja itakuwa hivyo.<br><br>Mimi hupendelea kutazama filamu za kutisha tofauti na dada yangu anayevutiwa na filamu za kuchekesha na zile zenye hadithi ndefu na mazungumzo mengi. Hivyo lazima nihakikishe kwamba filamu inayonivutia inaonyeshwa ndipo niende. Hii ni muhimu kwangu kwani kiingilio ni ghali na pia ninaishi nje ya mji hivyo jumba la sinema halipo karibu na nyumbani kwetu. |

**Simu za Mkononi**

**Question 4**

**Example**

**M1** Ninaitwa Mwamedi. Uzuri wa simu za mikononi ni mawasiliano mazuri.

**Question 4a**

**F1** Mimi ni Lola. Simu yangu ya mkono hufanya kazi vizuri mijini lakini ninapoenda vijijini haifanyi kazi.

**Question 4b**

**M2** Ninaitwa Mkude. Kuna simu za aina na bei tofauti kwa hivyo kila mtu ana uwezo wa kununua.

**Question 4c**

**F1** Jina langu ni Asha. Kuna watu ambao kamwe hawapokei simu zao za mkononi wanapopigiwa simu. Hukera sana.

**Question 4d**

**M1** Mimi ninaitwa Chege. Ni muhimu kuwa na simu ya mkononi hasa kwenye safari ndefu, lakini lazima kuzima mlio ili wasafiri wengine wasikereke.

**Question 4e**

**M2** Mimi ni Abushiri. Kuna michezo mingi kwenye simu za mkononi ambazo hufurahisha.

**Question 4f**

**M1** Mimi ni Kurwa. Vijana wengi hupoteza muda kwenye simu za mikononi.

## Taarifa ya Habari

**Question 5**

**Example**
**M1** Ninaitwa Amin na mimi hutazama taarifa ya habari kila siku.
**Question 5a**
**M1** Sivutiwi na taarifa za habari za nchini kwangu, mimi ninataka kujua mambo yanayotokea katika nchi nyingine duniani kote.
**Question 5b**
**M1** Mimi ninafikiri taarifa za habari ni muhimu sana. Nilipokuwa mdogo sikuweza kuzielewa vizuri kwani sikuwa na uelewa mzuri wa siasa za dunia.
**Question 5c**
**M1** Vijana wenzangu huniuliza kwa nini ninapenda kutazama kipindi ambacho kimejaa majanga ya kusikitisha tu.
**Question 5d**
**M1** Tofauti na wazazi wangu, mimi hupata taarifa ya habari kwenye mtandao, kwenye rununu au tarakilishi. Wao wanapendelea runinga ingawa wakati mwingine husikiliza radio.
**Question 5e**
**M1** Sitazami tarifa ya habari asubuhi kwa sababu hurudiwa rudiwa siku nzima kwa hivyo hakuna haja ya kusikiliza kila saa. Mimi husikiliza usiku kabla ya kulala.
**Question 5f**
**M1** Nitakapokwenda kusoma chuo kikuu nitasomea uandishi wa habari na kuweza kuwataarifu wananchi kuhusu miradi muhimu ya kujenga taifa letu.

**Mpira wa Miguu**

**Question 6**

| | |
|---|---|
| **M1** | Aaliyah, hivi mpira wa miguu ndio mchezo uupendao kuliko yote? |
| **F1** | Ndio. Mimi ninaupenda mpira wa miguu lakini hucheza mpira mara moja moja ninapopata nafasi ya kucheza. Nina bahati kwani nchini kwetu hali ya hewa ni ya joto kwa hivyo ni rahisi kucheza nje kwenye uwanja mkubwa. Kwa kawaida mimi hucheza jioni wakati jua linapozama. |
| **M1** | Wewe je Luka? |
| **M2** | Mimi pia ninapenda sana kucheza mpira wa miguu lakini mara nyingi hucheza mpira kwenye uwanja uliopo nyumbani kwetu. Zamani kaka yangu akipenda kucheza na mimi lakini siku hizi rafiki zangu huja kucheza na mimi. Mara nyingi mama hututahadharisha tusipige mpira kwenye eneo la nyanya zake zinazomea. |
| **M2** | Tuambie Zaidani, wewe unapenda mpira wa miguu pia? |
| M1 | Mimi ninapenda kutazama mpira wa miguu lakini si mchezaji. Sijawahi kuhamasishwa na kutamani kucheza. Lakini nimenunua shati la timu ya taifa ya mpira na huivaa ninapoenda mpirani. Mimi ni shabiki mzuri sana. |

## Usafiri

**Question 7**

| | |
|---|---|
| M1 | Je Salha, unapenda kutumia usafiri gani? |
| F1 | Kwa kawaida mimi hutumia basi ninapoenda shuleni kwa sababu nchini kwangu kuna barabara maalumu kwa ajili ya mabasi, kwa hivyo mimi hufika shuleni mapema sana. Siku zingine mabasi huchelewa na kunikera sana. |
| M1 | Vipi kuhusu usafiri wa gari moshi? |
| F1 | Hata watoto wadogo wanaweza kununua tiketi kirahisi na ofisi za tiketi huwa na punguzo la bei ingawa inabidi kujitayarisha kusimama kwa masaa. Hukereka pale ninapokuwa na tiketi lakini kulazimika kusimama njia nzima. |
| M1 | Je, wewe umewahi kusafiri na ndege? |
| F1 | Bila shaka. Ni raha sana kuwa ndani ya ndege na kuna idadi kadhaa tu ya wasafiri waliowekeza tiketi. Lakini kuna watu wengine wanachukizwa na utoaji wa hewa chafu unaofanywa na ndege. Hili ni jambo la kuangaliwa kwa makini sana. |
| M1 | Na pikipiki je? |
| F1 | Nilinunua pikipiki baada ya kufurahia kuwa popote ninapotaka kwa haraka sana. Hata kunyeshewa na mvua ninapokuwa kwenye pikipiki si mbaya sana. |
| M1 | Basi vizuri. |
| F1 | Asante. |

Pearson Education Limited. Registered company number 872828
with its registered office at 80 Strand, London, WC2R 0RL, United Kingdom